

# Nyumba ya Mungu ya kiroho “KANISA”

Wakristo  
Mawe yaliyo hai  
1 Petro 2:5


Yesu  
Mlango  
Yohana 10:9

Kweli  
1Timotheo 3:15

Mitume & manabii  
Msingi  
Waefeso 2:20

Juu ya mwamba huu  
nitalijenga kanisa langu  
Uungu wa Kristo  
Mathayo 16:13-18

Yesu, jiwe kuu  
la pembeni  
Waefeso 2:20



# Hatua kuelekea mbinguni

- **Sikia**

Yohana 6:45 = “imeandikwa katika manabii, na wote watakuwa wamefundishwa na Mungu. Basi kila aliyesikia na kujifunza kwa baba huja kwangu.”

- **Amini**

Yohana 8:24 = “kwa hiyo naliwaambieni ya kwamba mtakufa katika dhambi zenu; kwa sababu msiposadiki ya kuwa mimi ndiye, mtakufa katika dhambi zenu.”

- **Tubu**

Luka 13:3 = “nawaambia, sivyo; lakini msipotubu, ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo.”

- **Kiri**

Warumi 10:9-10 = “kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka.” Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.”

- **Batizwa**

Marko 16:16 = “Aminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa”

- **Ishi kwa uaminifu**

Ufunuo 2:10 = “Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima.”

